

TANGAZO LA KAZI ZA UJENZI

Tarehe: 09/03/2019

TANGAZO LA ZABUNI KWA AJILI YA MAFUNDI WAKUKAMILISHA WA UJENZI WA MADARASA MAWILI KATIKA SHULE YA SEKONDARI ITOBO

Halmashauri ya Wilaya ya Nzega imepokea fedha toka Serikali kuu kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba viwili vya madarasa katika shule ya sekondari Itobo kwa mwaka wa fedha 2018-2019

Kamati ya ujenzi ya shule ya sekondari Itobo inawatangazia Mafundi wote wa ujenzi wenye uwezo wa kukamilisha ujenzi wa vyumba hivyo kuomba kazi ya kukamilisha vyumba hivyo Halmashauri ya Wilaya ya Nzega katika shule ya sekondari Itobo.

Ukamilishaji wa vyumba hivyo hilo utafanyika kwa utaratibu wa kutumia "Force Account".

Sifa za mwombaji:-

- a. Muombaji awe na uzoefu wa kujenga majengo yanayofanana na kazi anayoomba (majengo ya serikali yatakuwa na faida zaidi) mwenye uangalizi mzuri wa mali wakati wa utekelezaji wa mradi huo.
- b. Muombaji ajue vyema kusoma ramani na vipimo vyake kwa ajili ya ufanisi wa kazi
- c. Muombaji aonyeshe mchanganuo wa muda wa utekelezaji mradi.
- d. Maombi yataendelea kuwa hai kwa muda wa siku 45 baada ya kufunguliwa.
- e. Muombaji awe na akaunti benki itakayowezesha malipo kwa njia ya hundi
- f. Kuwa na cheti cha ufundi ni sifa ya ziada.
- g. Muombaji awe na barua ya utambulisho wa eneo analotoka
- h. Muombaji awe na barua ya mdhamini kwa kazi husika

- i. Waombaji/Mafundi watatakiwa kuonesha kazi ambazo wamewahi kuzifanya pamoja na namba za simu za wateja wao waliowafanyia kazi hizo katika kipindi cha miaka mitatu (3) iliyopita.

Aidha kila mwombaji atatakiwa kuonyesha gharama za ufundi za ukamilishaji wa vyumba hivyo. Kazi zinazotarajiwa kufanyika ni pamoja na kuziba nyufa, kujaza kifusi, mawe na zege la jamvi, kujenga veranda, kuweka gypsum na kupaka rangi.

Mafundi watachaguliwa kwa kuzingatia sifa walizoambatanisha, gharama za ufundi pamoja na kuzingatia sheria na kanuni za Ununuzi wa Umma.

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 20 Machi, 2019 saa saba kamili mchana na waombaji wote wanatakiwa wawepo. Maombi yatakayochelewa baada ya muda tajwa hapo juu hayatapokelewa kwa ajili ya tathmini. Ufunguzi wa zabuni utafanyika mara baada ya muda wa kupokea zabuni kuisha.

Maombi yote yatumwe katika Ofisi ya Mkuu wa Shule, Shule ya Sekondari Itobo kwa anuani Ifuatayo:-

MKUU WA SHULE,
SEKONDARI YA ITOBO,
S. L. P 540,
ITOBO, NZEGA.

Gharama za maombi hayo ni shilingi 20,000.00 (elfu ishirini tu) ambazo hazitarudishwa.

Imeandaliwa na;


.....

BENSON M. JOHNSON
MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI ITOBO
NZEGA

HEADMASTER
ITOBO SECONDARY
P. O. BOX 540
NZEGA